JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2018

MKOA WA MTWARA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P 544
Simu: 023 2333014
Nukushi: 023 2333194
Barua pepe:ras@mtwara.go.tz
Tovuti: www.mtwara.go.tz

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Uongozi na wananchi wa Mkoa wa Mtwara tunayo furaha kubwa kuupokea Mwenge wa Uhuru. Tunayo matumaini makubwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2018, kwa kuwa tunatambua kazi kubwa inayofanywa na Mwenge wa Uhuru tangu kuwashwa kwake mwaka 1961.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Tunakukaribisha wewe, pamoja na wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa hapa Mkoani Mtwara. Tunawapongeza kwa kupewa dhamana kubwa ya kuukimbiza Mwenge wa Uhuru, tunawatakia kila la heri kwa Mwenyezi Mungu awalinde na mmalize mbio hizi salama salmin.

2.0 ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama Mkoani ni shwari na inaendelea kuimarika. Matatizo yanayojitokeza yameendelea kudhibitiwa na Vyombo vya Dola kwa kushirikiana na raia wema.

3.0 UTAWALA NA MAKAZI

Mkoa wa Mtwara una eneo la kilometa za mraba 16,720. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, unakadiriwa kuwa na watu 1,270,854. Kwa sasa Mkoa unakadiriwa kuwa na watu 1,356,802 kwa ongezeko la watu la asilimia 1.2 kwa mwaka. Watu wapatao 207,465 sawa na 23% wanaishi maeneo ya miji na watu 1,032,835 sawa na 77% wanaishi vijijini.

Kiutawala Mkoa umegawanyika katika Wilaya 5, Halmashauri 9, Tarafa 27, Kata 191, Mitaa 227, Vijiji 792, na Vitongoji 3,456 na una majimbo 10 ya Uchaguzi

4.0 HALI YA SIASA

Hali ya kisiasa Mkoani ni shwari na tuna jumla ya Vyama vya Siasa 11 vinavyofanya kazi za siasa. Aidha, Mkoa una Majimbo ya Uchaguzi kumi (10) ambayo ni (Mtwara Mjini, Mtwara Vijijini, Nanyamba, Tandahimba, Newala Mjini, Newala Vijijini, Masasi, Ndanda, Lulindi na Nanyumbu).

5.0 MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017.

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016/2017 zilianza rasmi tarehe 12 Mei, na kukimbizwa kwa siku 9 kwenye njia yenye urefu wa km 871.1 na kupitia jumla ya miradi 55 ambapo miradi 09 ilizinduliwa, miradi 07 ilifunguliwa, 18 iliwekwa mawe ya msingi na miradi 21 ilionwa na kukaguliwa yote ikiwa na thamani ya shilingi **17,736,208,261** (**Bilioni kumi na saba, milioni mia saba thelathini na sita, na laki mbili na nane mia mbili sitini na moja)** kwa mchanganuo ufuatao;

- **Mchango wa Wananchi** **shs. 1,806,008,400** **(10.2%)**
- **Mchango wa Halmashauri** **shs. 2,541,259,295.6** **(14.3%)**
- **Mchango wa Serikali Kuu** **shs. 8,040,242,267** **(45.3%)**
- **Mchango waWahisani** **shs. 5,348,698,298** **(30.2%)**

Aidha, Mbio hizo zilibeba ujumbe usemao "***Shiriki kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi yetu".*** Hadi kufikia Mei 2017 Mkoa wa Mtwara ulikuwa na viwanda vidogo 2,582 vilivyoajiri watu wapatao 19,190 na viwanda vikubwa 7 vilivyoajiri watu 2,805.

Aidha, Halmashauri na wadau wa maendeleo katika Mkoa wa Mtwara wameendelea kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya viwanda kuanzia viwanda vikubwa, vya kati na vidogo vidogo kwa kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji huo. Vile vile, Serikali kwa upande wake imeendelea na uimarishaji wa miundombinu mikubwa kama barabara za lami, upanuzi wa bandari, uwanja wa ndege ili kuvutia wawekezaji zaidi.

Sambamba na ujumbe huu, Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 zilibeba ujumbe wa kudumu juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Rushwa, Malaria na matumizi ya dawa za kulevya ukiwa umeainishwa kama ifuatavyo:

- Mapambano dhidi ya rushwa chini ya kaulimbiu ***"Tuungane kwa pamoja dhidi ya rushwa kwa maendeleo, amani na usalama wa Taifa letu".***
- Mapambano dhidi ya dawa za kulevya chini ya kaulimbiu***; "Tuwajali na tuwasikilize watoto na vijana"***
- Mapambano dhidi ya UKIMWI chini ya kaulimbiu ***"Tanzania bila maambukizi mapya, Unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana ifikapo mwaka 2030"***
- Mapambano dhidi ya Malaria chini ya kaulimbiu ***"Shiriki kutokomeza Malaria kabisa kwa manufaa ya jamii"***

6.0. MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018

Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2017/2018 utakimbizwa Halmashauri zote tisa kuanzia leo tarehe 11 Juni hadi 19 Juni, 2018 ambapo tutaukabidhi Mkoani Lindi katika Kijiji cha Madangwa.

Ukiwa Mkoani Mtwara Mwenge wa Uhuru utakimbizwa kwenye njia ya urefu wa **km 943** na kupitia jumla ya miradi 76 yenye gharama ya shilingi **29,571,290,632.00 (Bilioni ishirini na tisa, milioni mia tano sabini na moja, mia mbili tisini elfu,mia sita thelathini na mbili)** ambapo uchangiaji wake ni kama ifuatavyo;

- **Wananchi TSh. 594,061,470/= (2.01%)**
- **Halmashauri TSh. 2,283,201,433/= (7.72%)**
- **Serikali Kuu TSh. 18,294,199,929/= (61.86%)**
- **Wahisani TSh. 8,399,827,800/= (28.41%)**

Aidha, pamoja na kazi nyingine, Mbio za Mwenge wa Uhuru zitaweka mawe ya msingi miradi 28, kufungua miradi 10, kuzindua miradi 11 na kuona na kukagua miradi 27 inayotekelezwa na wananchi kwa kushirikiana na serikali, wahisanii na Halmashauri, hivyo, tunachukua fursa hii, kukuahidi kuwa tutashirikiana vyema na wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa katika kipindi chote watakapokuwa katika Mkoa wa Mtwara.

6.1. Utekelezaji wa Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru mwaka 2018

Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2018 zimebeba ujumbe unaojikita katika kuwahamasisha wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **kuwekeza katika elimu** chini ya kaulimbiu isemayo: ***"Elimu ni ufunguo wa Maisha; Wekeza sasa kwa Maendeleo ya Taifa Letu***". Ujumbe ambao Mkoa wa Mtwara kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo tunautekeleza kwa vitendo.

- **Taasisi za elimu Mkoa wa Mtwara**

Mkoa una jumla ya shule za msingi 667 (za serikali 660 na zisizo za serikali 7), za sekondari zikiwa 147 (135 za serikali na 12 zisizo za serikali) na za msingi ni 520. Aidha, kutokana na sera ya elimu inayotaka kuwepo kwa madarasa ya awali katika kila shule ya msingi, Mkoa una jumla ya madarasa 670 ya elimu ya awali.

Aidha, katika kuhakikisha watoto na vijana wa Mtwara wanaendelea kupata ujuzi na stadi, Mkoa una jumla ya shule 11 zinazotoa elimu ya ufundi stadi, shule 14 zenye vitengo vya elimu maalumu, vituo vya walimu

27 (TRCs), Vyuo vya ualimu 4 (Serikali 3 na visivyo vya serikali 1), Vyuo vya maendeleo ya wananchi 3, Chuo cha VETA 1, Vyuo vinavyotoa mafunzo ya ufundi (VET Providers) 4 na Vyuo vikuu 2.

- **Uandikishaji wa wanafunzi shuleni na upatikanaji wa elimu kwa wote**

Mkoa umeendelea kuongeza kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali ambapo kwa mwaka 2017 jumla ya wanafunzi 41,665 waliandikishwa na mwaka 2018 wanafunzi 41,678 wameandikishwa sawa na ongezeko la asilimia 0.03. Kwa upande wa elimu msingi uandikishaji kwa mwaka 2017 ulifikia wanafunzi 54,553 na mwaka 2018 wanafunzi 45,401 sawa na asilimia 100 ya maoteo . Na kiwango cha wanafunzi wa sekondari wanaojiunga na kidato cha kwanza kimeongezeka kutoka wanafunzi 13,123 kwa mwaka 2017 hadi wanafunzi 16,639 kwa mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 26.79.

- **Rasilimali watu katika sekta ya elimu**

Mkoa wa Mtwara unao utoshelevu na ziada ya walimu wa masomo ya sanaa katika shule za sekondari na kutokana na ziada hiyo jumla ya walimu 360 wa masomo ya sanaa wamehamishiwa shule za msingi ili kuondoa tatizo la walimu. Hata hivyo, pamoja na hatua hii nzuri Mkoa bado una upungufu wa walimu 764 wa masomo ya sayansi, hisabati na biashara kwa shule za sekondari ikilinganishwa na mahitaji ya walimu 1252 yaliyopo sasa. Hata hivyo, Mkoa kwa kushirikiana na wananchi umeendelea kutumia mbinu mbalimbali za upatikanaji wa walimu hao ikiwa ni pamoja na kutumia wanavyuo wa kujitolea wa masomo ya sayansi na hisabati kutoka Vyuo Vikuu vilivyoko Dodoma wenye asili ya Mikoa ya Mtwara na Lindi na wasomi wengine wa kujitolea ndani ya Mkoa.

- **Uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia**

Mkoa wa Mtwara umekuwa mstari wa mbele kuhakikisha unamaliza kabisa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa 3,032, nyumba za walimu 5,308 na matundu ya vyoo 6,674 kwa kutekeleza mikakati kadhaa ikiwa ni pamoja na kuanzisha benki ya matofali kwa kila Kijiji, kuendelea na ujenzi wa madarasa mapya 82 (27 ya EP4R na 55 ya mpango wa Mkoa wa uboreshaji wa shule zenye uhaba mkubwa wa madarasa), ujenzi wa mabweni 10, matundu ya vyoo 64 na ukarabati wa majengo 7 ya shule za sekondari na 2 ya shule za msingi. Kwa ujumla ujenzi wa miundombinu hii imegharimu shilingi 4,002,743,116.33 (**Bilioni nne, na milioni mbili, laki saba arobaini na tatu, mia moja kumi na sita na senti thelathini na tatu**) ambapo kati ya fedha hizo shilingi 3,860,505,433.00 ni za mpango wa EP4R na shilingi 142,237,683.33 za Mpango wa Mkoa wa uboreshaji wa shule zenye uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa. Aidha, kati ya

shilingi 142,237,683.33 Wananchi wamechangia shilingi 102,237,683.33 na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara imechangia shilingi 40,000,000/=

- **Utekelezaji wa dhana ya elimu msingi na sekondari bure**

Wananchi wa Mkoa wa Mtwara wamepokea kwa mwitikio mzuri dhana ya Elimu Bure ambayo imepelekea kupanda kwa uandikishaji wa wanafunzi kwa shule za Msingi na Sekondari. Kuanzia Julai 2017 hadi Mei 2018 Mkoa umepokea fedha za ruzuku shilingi **8,073,600,012/=** kwa shule za msingi na shilingi **9,564,528,000/=** kwa shule za sekondari sawa na asilimia 100. Hata hivyo, wananchi wa Mkoa wa Mtwara wameendelea kutekeleza wajibu wao katika kuunga mkono dhana hii kwa kuchangia ujenzi wa miundombinu ya shule na utoaji wa huduma ya chakula kwa watoto shule zote za msingi na sekondari kwa kushirikiana na kamati na bodi za shule.

Vile vile, kupitia mradi wa Tusome Pamoja jumla ya Waelimishaji Jamii (WJE) 1,326 wamebainishwa na kufanyakazi ya kuhamasiha jamii na rasilimali mbalimbali katika uboreshaji elimu. Aidha, Umoja wa Wazazi na Walimu (UWAWA) umeanzishwa kwa shule 663 za msingi za Mkoa wa Mtwara kwa lengo la kusaidia uendeshaji wa shule za msingi, kuhamasisha jamii kusimamia na kufuatilia ujifunzaji na ufundishwaji wa watoto shuleni na uboreshaji wa sekta nzima ya elimu.

- **Uhamasishaji wa masomo ya sayansi**

Katika jitihada za kuwekeza kwenye masomo ya sayansi na hisabati, Mkoa umejenga jumla ya maabara 405 katika shule za sekondari 135 ambazo ni sawa na asilimia 33.33. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya maabara 326 sawa na asilimia 80.49 zimepokea vifaa vya maabara na shule 79 sawa na asilimia 19.51 bado hazijapokea vifaa vya maabara.

Sambamba na ujumbe wa Mwenge mwaka 2018, Mbio za Mwenge wa Uhuru zimebeba ujumbe wa kudumu kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa, UKIMWI, Malaria na Dawa za Kulevya kama ifuatavyo;

- Mapambano dhidi ya rushwa chioni ya kaulimbiu **"Kataa Rushwa- Jenga Tanzania"**
- Mapambano dhidi ya UKIMWI chini ya kaulimbiu **" Mwananchi jitambue; Pima afya yako sasa"**
- Mapambano dhidi ya Malaria chini ya kaulimbiu **"Shiriki kutokomeza Malaria kwa manufaa ya jamii"**

- Mapambano dhidi ya dawa za kulevya chini ya kaulimbiu " **Tuwasikilize na kuwashauri watoto ili wasitumie dawa za kulevya"**

Kwa ujumla Mkoa umejipanga vyema na unaendelea kupambana na mambo yote hayo manne kama yatakavyooneshwa wazi katika taarifa za Wilaya na miradi itakayopitiwa na Mwenge wa Uhuru.

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018 MKOA WA MTWARA

TAREHE	MUDA	MAHALI	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
11/06/2018	02:30 - 03:30	Lumesule	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kimkoa na Halmashauri	RC Mtwara/RC Ruvuma/DC Nanyumbu
12/06/2018	03:00 – 03:30	Mkarakate	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Mji Masasi	DC Masasi
13/06/2018	02:30 – 03:30	Mpeta	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	DC Masasi
14/06/2018	02:30 – 03:30	Moneka	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Mji Newala	DC Newala
15/06/2018	02:00 – 04:30	Mkwedu	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Newala	DC Newala
16/06/2018	02:30 – 04:00	Lidumbe Mtoni	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	DC Tandahimba
17/06/2018	02:00 – 03:00	Chikwaya	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Mji Nanyamba	DC Mtwara
18/06/2018	02:00 – 03:00	Mtama	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	DC Mtwara
19/06/2018	02:30 – 03:30	Mikindani	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani	DC Mtwara
20/05/2018	02:00 – 03:00	Madangwa	Makabidhiano ya Mwenge Mkoa wa Mtwara na Lindi	RC Mtwara/RC Lindi

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
11/06/2018	02.30- 03.50	Lumesule	00	Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kutoka ngazi ya Mkoa/Wilaya	RC Mtwara/ RC Ruvuma/ DC Nanyumbu
	03:50 – 04:10	*Lumesule*	*21.8*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Makong'ondera*	*DC*
	04:10 – 05:20	Makong'ondera		• Kukimbiza Mwenge • Kufungua Ofisi ya Kijiji cha Makong'ondera • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chai**	DC
	05:20 – 05:35	*Makong'ondera*	*25*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Nakopi*	DC
	05:35 – 06:00	Nakopi		• Kukimbiza Mwenge • Kuzindua mradiwa umeme jua • Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa soko la Kijiji	DC
	06:00 – 06:15	*Nakopi*	*15*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Likokona*	*DC*
	06:15 – 06:33	Likokona		• Kukimbiza Mwenge • Kuzindua nyumba ya kuishi walimu shule ya sekondari Likokona	DC
	06:33 – 07:00	*Likokona*	*27*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Nahawara*	*DC*
	07:00 – 08:15	Nahawara		• Kukimbiza Mwenge • Kuzindua madarasa 4, Ofisi 2 za walimu na matundu 10 ya vyoo • Kugawa madawati 560 kwa shule za Msingi • **Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru** • **Chakula cha mchana**	DC
	08:15 – 08:20	*Nahawara*	*12*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Chipuputa*	*DC*
	08:20 - 08:38	Chipuputa		• Kukimbiza Mwenge • Kufungua majengo ya zahanati ya Kijiji cha Chipuputa	DC
	08:38 – 09:05	*Chipuputa*	*30*	*Msafara wa Mwenge kuelekea*	*DC*

				Nagomba	
	09:05 – 09:30	Nangomba		• Kukimbiza Mwenge • Kufungua maabara 3 za sayansi shule ya sekondari Nangomba • Kukabidhi viti na meza 953 kwa shule za sekondari za Wilaya ya Nanyumbu	*DC*
	09:30 -09:40	*Nangomba*	*15*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Kilimanihewa*	*DC*
	09:40 – 11:30	Kilimahewa		• Kuona na kukagua shughuli za vijana na wanawake wajasiriamali na kutoa mikopo • Kuona na kukagua banda TAKUKURU na klabu za wapinga rushwa • Kuona na kukagua banda la afya na mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kugawa vyandarua kwa WAVIU na kadi za CHF kwa wazee • Kuona na kukagua banda la elimu na kutoa zawadi ya baskeli 12 kwa wanafunzi wa sekondari wenye mazingira magumu • **Risala ya utii** • Burudani • **Ujumbe wa Mwenge** • **Mkesha**	DC
12/06/2018	11:00 – 01:30	Mangaka	00	Chai na kuaga wananchi	DC
	01:30 – 02:30	*Mangaka*	*40*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Mkarakate*	*DC*
	02:30 – 03:30	Mkarakate		Kukabidhi Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Mji Masasi	DC
			186.8		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA MJI MASASI.

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
12/06/2018	2.00 - 3.00	MKARAKATE	km 0	• Halmashauri ya Mji Masasi kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa viongozi wa Wilaya ya Nanyumbu.	Mkuu wa Wilaya
	03:00- 03:05	Mkarakate	4	Msafarawa Mwenge kuelekea Sululu	
	03.05 -04.05	SULULU		• Mwenge utakimbizwa • Kufungua klabu ya rushwa Sekondari Ya Sululu • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chai**	- do- - do- - do- - do-
	04:05-04:10	Sululu	2	Msafara wa Mwenge kuelekea Songambele	
	4.10 - 4.40	Songambele		• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi mradi wa Maji	- do-
	4:40 – 4:45	Songambele	6	Msafara wa Mwenge kuelekea Maendeleo	
	4.45 - 5.25	Maendeleo		• Kuona na kukagua mafunzo ya TEHAMA shule ya msingi Maendeleo • Kuona na kukagua utolewaji wa chakula shule ya Msingi Maendeleo.	- do-
	5:25 – 5:30	Maendeleo	2	Msafara wa Mwenge Kuelekea Mkomaindo	
	5.30 – 6:00	MKOMAINDO		Kufungua mradi wa Barabara	- do-
	6:00 – 6:05	Mkomaindo	0.5	Msaafara wa Mwenge kuelekea Hospitali ya Mkomaindo	
	6:05 – 6:30	MKOMAINDO		Kufungua mradi wa Duka la Dawa	- do-
	6:30 – 6:45	Mkomaindo	19	Msafara wa Mwenge Kuelekea Mumbaka	
	6:45-7:15	MUMBAKA		Kuweka jiwe la Msingi chumba cha kujifungulia Zahanati ya Mumbaka	- do-
	7:15 – 7:30	Mumbaka	19	Msafara wa Mwenge kuelekea COTC	
	7:30 – 8:15	COTC		**Chakula cha mchana**	- do-
	8:15 – 8:20	COTC	3	Msafara wa Mwenge kuelekea	

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
				Mkuti	
	8:20 – 9:00	MKUTI		• Mwenge utakimbizwa • Kukabidhi hundi za mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake • Kuona na kukagua mabanda ya wajasiliamali • **Ujumbe wa Mwenge**	
	9:00 – 9:15	Mkuti	13	Msafara wa Mwenge kuelekea Magumchila	
	9.15 – 9:45	MAGUMUCHILA		● Kuweka jiwe la Msingi vyumba 6 vya madarasa, ofisi ya walimu na Nyumba za walimu s/m Magumuchila	- do-
	9:45 – 10:00	Magumuchila	16	Msafara wa Mwenge kuelekea uwanja wa Napupa	
	10:00	UWANJA WA NAPUPA		• Mwenge utakimbizwa • Kuona na kukagua na kupata taarifa zinazohusiana na:- o UKIMWI o Rushwa o Malaria o Madawa ya kulevya • **Risala ya utii** • **Ujumbe wa Mwenge** • **Mkesha wa Mwenge**	
13/6/2018	12.00 - 1.00	COTC	0	CHAI na kuaga wananchi	Mkuu wa Wilaya
	1:00 – 1:45	Napupa	43.8	Msafara wa Mwenge kuelekea Mpeta	
	1.45 – 3:00	MPETA		Kukabidhi Mwenge kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.	
			128		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
13/6/2018	03. 00 - 04.00	Mpeta	0	Halmashauri ya wilaya ya Masasi kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa uongozi wa H/Mji Masasi	Mkuu wa wilaya
	04:00 – 04:10	*Mpeta*	*8*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Chiungutwa*	*DC*
	04.10 – 05.10	Chiungutwa		• Mwenge Utakimbizwa • Kutoa Hundi za Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake na Vijana • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chai**	DC
	05:10 – 05:40	*Chiungutwa*	*21*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Ndwika*	*DC*
	05.40 – 06.25	Ndwika		• Mwenge utakimbizwa • Kuweka Jiwe la Msingi Mradi wa ujenzi wa Maabara ya Geography, madarasa 7, Mabweni 2 na Jengo la Utawala	DC
	06:25 – 06:35	*Ndwika*	*7*	*Masafara wa Mwenge kuelekea Nagaga*	*DC*
	06.35 –07. 05	Nagaga		• Mwenge utakimbizwa • Kuweka Jiwe la Msingi Mradi wa Ujenzi wa Jengo la upasuaji, Wodi ya wazazi, Maabara, jengo la kuhifadhi Maiti na Nyumba ya Mtumishi	DC
	07:05-07:35	*Nagaga*	*21*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Namombwe*	*DC*
	07.35 - 08.50	Namombwe		• Mwenge utakimbizwa • Kuzindua klabu ya wapinga Rushwa Shule ya Sekondari Namombwe • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chakula cha mchana**	DC
	08:50-09:05	*Namombwe*	*13*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Mkwaya*	*DC*
	9.05– 9.30	Mkwaya		• Mwenge Utakimbizwa • Kuweka jiwe la Msingi mradi wa Maji Rivango --	DC

				Makong,onda	
	09:30-09.40	*Mkwaya*	*10*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Mnavira*	*DC*
	09:40	Mnavira		• Mwenge wa utakimbizwa • Kuweka Jiwe la Msingi Ujenzi wa Madarasa 3 S/Msingi Mnavira • **Risala ya utii** • **Ujumbe wa Mwenge** • **Mkesha wa Mwenge**	
14/6/2018	12:30 – 02:00	Mnavira	0	Chai ya asubuhi na Kuaga wananchi	DC
	02:00- 02:20	Mnavira	18	Msafara wa Mwenge kuelekea Moneka	DC
	02:20 – 04:00	Moneka		Kukabidhi Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Mji Newala	DC Masasi & DC Newala
			98		

RATIBA YA NJIA YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA MJI NEWALA

TAREHE	MUDA	MAHALI	KM	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
14/06/2018	3:00-4:00	Moneka	0.0	Kupokea Mwenge kutoka Halmashauri ya wilaya Masasi.	DC
	4:00-4:04	Moneka	1.5	Mwenge wa Uhuru kuelekea barabara ya Newala-Mbuyuni	DC
	4:04-4:15	Moneka		Kuweka jiwe la msingi barabara ya Newala-Mbuyuni kilomita 1.3 kwa kiwango cha lami.	DC
	4:15-4:19	Nangwala	2.0	Msafara wa Mwenge kuelekea Newala Day - Nangwala	DC
	4:19-5:30	Nangwala		• Kukimbiza Mwenge . • Kugawa madawati kwa shule za sekondari Newala. • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chai.**	DC
	5:30-5:36	NANGWALA CHINI	3.0	Mwenge kuelekea Amkeni ujenzi	DC
	5:36-5:52	Amkeni		• Kukimbiza Mwenge . • Kuona/kukagua ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi.	DC
	5:52-5:57	Amkeni	2.5	*Mwenge wa Uhuru kuelekea Mtangalanga*	DC
	5:57-6:20	Mtangalanga		• Kukimbiza Mwenge • Kuona/kukagua Elimu kwa vitendo (practical) maabara ya Shule ya Sekondari Mtangalanga.	DC
	6:20-6:35	Mtangalanga	10	*Mwenge wa Uhuru kuelekea Nambunga*	DC
	6:35-7:05	Nambunga		• Kukimbiza Mwenge . • Kuzindua Club ya wapinga Rushwa. • Kuzindua madarasa 2 na ofisi 1, Shule ya Sekondari Nambunga	DC
	7:05-7:23	Nambunga	12.5	*Mwenge wa Uhuru kuelekea Namiyonga .*	DC

	7:23-8:43	Namiyonga		• Kukimbiza Mwenge . • Kuona vikundi vya wajasiliamali wanawake na vijana. • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chakula cha mchana.**	DC
	8:43-9:00	Namiyonga	9	• *Mwenge wa Uhuru kuelekea Kiuta*	DC
	9:00-9:15	Kiuta		• Kukimbiza Mwenge . • Kuweka jiwe la msingi bwalo la chakula shule ya sekondari Kiuta.	DC
	9:15-9:21	Kiuta	6.0	*Mwenge wa Uhuru kuelekea Mnalale*	DC
	9:21-9:36	Mnalale		• Kukimbiza Mwenge . • Kuweka jiwe la msingi nyumba ya mwalimu shule ya msingi Mnalale.	DC
	9:36-10:12	Mnalale	23	*Mwenge wa uhuru kuelekea Newala Mjini*	
	10:12-	Newala mjini		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kupata taarifa juu ya mapambano dhidi ya Rushwa, Malaria, Ukimwi na Dawa za kulevya. • Risala ya utii • Burudani • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chakula cha jioni** • **Mkesha wa Mwenge**	DC
15/06/2018	12:00-1:50	Newala mji	0.0	• Chai ya asubuhi na kuaga wananchi	DC
	1:50-2:18	Newala Mjini	14	*Mwenge kuelekea Mkwedu.*	DC
	2:18-2:25	Mkwedu		Kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Halmashauri ya wilaya Newala.	DC
			83.5		

RATIBA YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

TAREHE	MUDA	MAHALI	KM	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
15/6/2018	03:00 - 04:00	Mkwedu		Kupokea Mwenge kutoka Halmashauri ya Mji Newala	DC Wananchi
	04:00 - 04:15	*Mkwedu*	*10*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Makukwe*	*DC*
	04:15 - 04:45	Makukwe		• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la Msingi vyumba 5 vya madarasa	DC
	04:45- 04:55	*Makukwe*	*4*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Mtunguru*	*DC*
	04:55 - 05:55	Mtunguru		• Kukimbiza Mwenge • Kuzindua klabu ya Wapinga Rushwa Shule ya Msingi Mtunguru • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chai**	DC
	05:55- 06:15	*Mtunguru*	*9*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Lengo*	*DC*
	06:15 - 06:50	Lengo		• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la Msingi nyumba ya walimu 6 in1	DC
	06:50 - 07:15	*Mchemo A*	*21*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Mtopwa*	*DC*
	07:15 - 8:50	Mtopwa		• Kukimbiza Mwenge • Kukagua na kuona shughuli za vikundi vya Vijana na Wanawake vya uzalishaji mali • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chakula cha mchana**	DC
	08:50 - 09:20	*Maputi*	*22*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Maputi*	*DC*
	09:20-09:50	Maputi		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua Upanuzi wa Miundo-mbinu ya Chuo cha Ualimu Kitangali.	DC
	09:50-09:55	*Maputi*	*5*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Kitangari*	*DC*
	09:55-10:25	Kitangari		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na Kukagua mradi wa upanuzi wa miundo mbinu ya	DC

				Kituo cha Afya Kitangali	
	10:25-10:30	*Kitangari*	*1*	*Msafara kuelekea eneo la mkesha Kitangari*	*DC*
				• Kukimbiza Mwenge • Kuona juhudi za Halma shauri za kupambana na UKIMWI, Madawa ya kulevya, Rushwa na Malaria. • Risala ya utii • **Ujumbe wa Mwenge** • **Mkesha** • **Chakula - jioni**	
16/06/2018	12:00 - 01:00	Kitangari	0.0	Chai na kuaga wananchi	DC
	01:05 – 01:20	*Kitangari*	*30*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Lidumbe Mtoni*	*DC*
		Lidumbe Mtoni		Kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	DC Newala na DC Tandahimba
			102		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017
WILAYA YA TANDAHIMBA

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI KM	SHUGHULI/TUKIO	MHUSIKA
	12:30 – 3:30	LIDUMBE MTONI	0.0	Mapokezi Mwenge wa Uhuru Kutoka Wilaya ya Newala	DC
	3.30 - 3.35			Mwenge wa uhuru kuelekea Mahuta	Mkuu wa Wilaya
	3:35 – 3:50	MAHUTA MJINI	3	• Mwenge wa uhuru utakimbizwa • **KUWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA UJENZI NA UKARABATI WA MAJENGO YA KITUO CHA AFYA MAHUTA**	Mkuu wa Wilaya
	3:50 - 4:05	Mahuta	12	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Kijiji cha Nanhyanga	DC
	4:05 – 5:05	Nanhyanga		• **Mwenge wa uhuru Utakimbizwa** • **KUWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA MADARASA MAWILI NA OFISI MOJA SHULE YA SEKONDARI NANHYANGA.** • **CHAI YA ASUBUHI SEKONDARI YA NANHYANGA**	Mkuu wa Wilaya.
	5:05-5:08	Nanhyanga	2	Mwenge wa uhuru kuelekea stendi - Nanhyanga	
	5:08-5:28	NANHYANGA STEND		• **Mwenge wa uhuru utakimbizwa.** • **KUWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA KITUO CHA MABASI NANHYANGA** • **Ujumbe wa Mwenge**	
	5:28 – 5:38	Nanhyanga stendi	12	Mwenge wa Uhuru kuelekea Malopokelo	
	5:38 – 5:53	MALOPOKELO		• **Mwenge wa uhuru utakimbizwa.** • **KUZINDUA MRADI WA NYUMBA 6 ZA WAALIMU SEKONDARI YA TANDAHIMBA**	Mkuu wa Wilaya
	5:55 – 5:58	Malopokelo		Mwenge wa uhuru kuelekea Matogoro	

	5:55 - 6:10.	Matogoro		• **Mwenge wa uhuru utakimbizwa** • **KUWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA KITUO CHA MAARIFA/UFUNDI – MATOGORO**	Mkuu wa Wilaya
	6:10-6:16	Matogoro	2	Mwenge wa uhuru kuelekea Shule ya Msingi Maalum - Mji Mpya	Mkuu wa Wilaya
	6:16-6.31	Mji Mpya		• **Mwenge wa uhuru utakimbizwa.** • **Kufungua bweni 1 la Wasichana Shule ya Msingi Mji Mpya Maalum**	Mkuu wa Wilaya
	6.31-6.35	Mji Mpya	1	Mwenge wa uhuru kuelekea Ukumbi wa Halmashauri	Mkuu wa Wilaya
	6.35 – 8:10	Ukumbi wa Halmashauri		• Mwenge wa uhuru utakimbizwa • Taarifa ya mikopo ya vikundi vya vijana na wanawake. • Kuona na kukagua shughuli za wajasilia mali • **UJUMBE WA MWENGE** • **CHAKULA CHA MCHANA**	Mkuu wa Wilaya
	8:10 – 8:25	Ukumbi wa Halmashauri	18	Mwenge wa uhuru kuelekea Nachunyu.	Mkuu wa Wilaya
	8:25-8:40	Nachunyu		• **Mwenge wa uhuru utakimbizwa** • **KUWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI NACHUNYU.**	
	8:40-9.20	Nachunyu	18	Mwenge wa Uhuru kuelekea Luagala	

	9:20	Luagala		Mwenge Utakimbizwa • Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa matundu ya vyoo 32 shule ya msingi luagala. • Kuona na kukagua ujenzi wa kisima 1 lita 100,000 na ukarabati wa vyumba vya madarasa vinane (08). • Kupata taarifa ya mapambano dhidi o malaria (ugawaji vyandarua kwa wanafunzi/wajawazito) o Rushwa o UKIMWI o madawa ya kulevya • **Risala ya utii** • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chakula cha jioni luagala mission** • **Mkesha wa Mwenge wa uhuru-Luagala**	Mkuu wa Wilaya Mkuu wa Wilaya
17/6/2018	12:00 – 1:00	Luagala	0	Chain na kuwaaga Wananchi	DC
	1:00 – 2:00	Luagala	45	Msafara wa Mwenge kuelekea Chikwaya	DC
	2:00 – 3:00	Chikwaya	0	Kukabidhi Mwenge wa Uhuru wilaya ya Mtwara.	DC tandahimba na DC Mtwara
			113		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI KM	SHUGHULI/TUKIO	MHUSIKA
17/06/2018	02:15-03:00	Chikwaya	0.0	-Kupokea Mwenge wa uhuru Kutoka Halmashauri ya Wilaya Tandahimba	DC Tandahimba na DC Mtwara
	03:00-03:20	Chikwaya	0.1	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi ujenzi nyumba ya walimu 2 in 1 Shule ya msingi Chikwaya	
	03:20-03:25	*Chikwaya*	*2*	*Msafara wa Mwenge kuelekea shule ya sekondari Dinyecha*	*DC*
	03:25-03:50	Chikwaya		• Kukimbiza Mwenge • Kuweka Jiwe la msingi ujenzi madarasa 3 shule ya sekondari Dinyecha	
	03:50-04:00	*Chikwaya*	*3.1*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Shule ya Msingi Dinyecha*	*DC*
	04:00-05:30	Dinyecha S/M		• **Chai** • **Ujumbe wa Mwenge**	
	05:30-05:45	*Dinyecha S/M*	*10*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Chiwilo*	*DC*
	05:45-06:15	Chiwilo		• Kukimbiza Mwenge • Kuweka Jiwe la Msingi ujenzi wa madarasa 4 na vyoo matundu 6	
	06:15-06:35	Chiwilo	15.8	Msafara wa Mwenge kuelekea Majengo	
	06:35- 8:00	Majengo		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya Majengo • **Ujumbe wa Mwenge** • **Chakula cha Mchana**	
	08:00-08:15	*Majengo*	*12*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Hinju*	*DC*
	08:15-08:45	Hinju		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua vikundi vya ujasiriamali vijana na wanawake	DC
	08:45-08:55	*Hinju*	*8*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Nanyamba*	*DC*

	08:55-09:25	Nanyamba		• Mwenge kukimbizwa • Kuona na kukagua ujenzi wa Jengo la Utawala	DC
	09:25-09:40	*Nanyamba*	*4*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Nanyamba sekondari*	*DC*
	09:40-10:10	Nanyamba sekondari		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua maandalizi ya Miundo mbinu ya kidato cha Tano na Sita shule ya Sekondari Nanyamba	DC
	10:10-10:15	*Nanyamba sekondari*	*2*	*Msafara wa Mwenge kuelekea viwanja vya shule ya msingi Nanyamba*	*DC*
	10:15-	Shule ya msingi Nanyamba		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua mabanda ya mapambano dhidi ya Rushwa, Mapambano dhidi ya Malaria, VVU/UKIMWI • **Risala ya utii** • **Ujumbe wa Mwenge** • **Mkesha**	
18/06/2018	12:00-01:45	S/M Nanyamba		Chai na kuaga wananchi	DC
	01:45-02:30	*S/M Nanyamba*	*16*	*Msafara wa Mwenge kuelekea Mtama*	*DC*
	02:30-03:00	Mtama		Kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	Mkurugenzi Nanyamba TC na Mkurugenzi Mtwara DC
			73		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA WILAYA MTWARA

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
18.06.2018	2.30 – 3.00	Mtama	KM 0	Kupokea Mwenge wa uhuru kutoka Halmashauri ya Mji Nanyamba	DC
	3.00 – 3.30	Mtama		Ufunguzi wa nyumba ya Mtumishi Zahanati ya Mtama.	DC
	3.30 – 3.50	Namuhi	KM 20	Msafara kuelekea Namuhi	DC
	3.50 – 4.20	Namuhi		Uzinduzi wa daraja linalounganisha Vijiji vya Namuhi na Mnyija	DC
	4.20 – 4.30	Namuhi	KM 6	Msafara kuelekea Libobe Sekondari.	DC
	4.30 – 6.00	Libobe Sec.		• Ufunguzi wa madarasa 2, kutembelea na kukagua ujenzi wa maabara ya Fizikia pamoja na kukabidhi madawati 1,000 kwa Shule za sekondari 11. • **Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru** • **Chai**	DC
	6.00 – 6.30	Libobe Sec.	KM 12	Msafara kuelekea Nanyani	DC
	6.30 – 7.30	Nanyani		Uwekaji wa jiwe la msingi madarasa 6, na Ofisi 1 Shule ya Msingi Nanyani	DC
	7.30 – 7.50	Nanyani	KM 7.7	Msafara kuelekea Lyowa	DC
	7.50 – 8.30	Lyowa-Muungano		Kuzindua barabara ya km 4.7 iliyotengenezwa kwa nguvu za wananchi	DC
	8.30 – 8:40	Muungano	KM13	Msafara kuelekea Likonde	DC
	8:40 – 9:20	Likonde		• **Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru** • **Chakula cha mchana**	DC
	9.20 – 9.25	Likonde	KM 1	Msafara kuelekea Hiyari	DC
	9.25 – 9.55	Hiyari		Kuona na kukagua Mradi wa kufua umeme “power plant” Kijiji cha Hiyari.	DC
	9:55 – 10.00	Hiyari	KM 2	Msafara kuelekea eneo la mabanda ya ujasiriamali - Hiyari	DC
	10.00 – 10.30	Hiyari		Kuona na kukagua mabanda ya wajasiriamali Vijana na wanawake Kijiji cha Hiyari.	DC
	10.30 – 10.35	Hiyari	KM 3	Msafara kuelekea Kijiji cha msijute	DC
	10.35	Msijute		• Ukaguzi mabanda ya mapambano	DC

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
				dhidi ya o Rushwa, o madawa ya kulevya, o malaria na o UKIMWI • **Kusoma Risala ya utii** • **Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru** • **Mkesha wa Mwenge wa Uhuru**	
19.06.2018	12:00– 1:00	Msijute		Chai na kuaga Wananchi	DC
	1:00 – 2:00	Msijute	Km 5	Msafara kuelekea eneo la makabidhiano - Mikindani	DC
	2:00 – 3:00	Mikindani		Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kati ya Halmashauri ya wilaya ya Mtwara na Manispaa ya Mtwara - Mikindani	DC
			69.7		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018
HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA MIKINDANI.

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI KM	SHUGHULI/TUKIO	MHUSIKA
19/6/2018	1:30 – 3:25	Mikindani Stendi		• Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. • Kuona na kukagua mradi wa ukarabati wa gereza la kale	MD na DED
	3:30 – 3:35	Mikindani stendi	0.5	Msafara kuelekea makumbusho ya Dr. Livingstone	
	3:35 – 5:00	Magengeni		• Kuona na kukagua makumbusho ya Dr. Livingstone yaliyopo Magengeni • Kukagua vikundi vya wajasiliamali (wachoraji na wachongaji) • **Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru** • **Chai**	
	5:00 – 5:10	Magengeni	12.5	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Shangani	
	5:10 – 5:30	Shangani		• Kuweka Jiwe la Msingi ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Idara • Kugawa Pikipiki 4 kwa Watendaji wa Kata.	
	5:30 – 5:35	Shangani	3.7	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mtaa wa Rahaleo	
	5:35 – 6.15	Rahaleo		• Kuweka Jiwe la Msingi ujenzi wa Kituo cha wajasiliamali • Kukagua na kuona vikundi vya wajasiliamali • Kugawa hundi za mikopo kwa wajasiliamali • Kugawa vyerehani kwa vikundi vya wanawake na Vijana. • **Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru**	
	6:15 – 6:20	Rahaleo	1.2	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Vigaeni	
	6:20 – 6:40	Vigaeni		Kuweka jiwe la ufunguzi wa maabara ya vifaa vya ujenzi	
	6:40 – 6:45	Vigaeni	2	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Michael Arch Angel - Shangani	
	6:45 – 7:15	Shangani		• Kuona na kukagua Mchango wa	

				Sekta Binafsi katika uwekezaji katika Elimu • Kugawa zawadi kwa shule zilizofanya vizuri kielimu	
	7:15 – 7:20	Shangani	1.4	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Police Officers Mess – Shangani.	
	7:20 – 8:20	Shangani		**Chakula cha Mchana**	
	8:20 – 8:25	Shangani	5.2	Msafara kuelekea Likombe	
	8:25 – 8:45	Likombe		Kuona na kukagua kiwanda cha kubangua korosho cha MICRONIX	
	8:45 – 8:50	Likombe	1.8	Msafara kuelekea Kituo cha Afya - Likombe	DC
	8:50 – 9:20	Likombe		• Kuweka jiwe la msingi upanuzi wa Kituo cha Afya Likombe • Kugawa kadi za CHF kwa wazee na watoto • Kugawa vyandarua kwa wanawake wajawazito	
	9:20 – 9:30	Likombe	7.2	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mtawanya	
	9:30 – 10:00	Mangamba		• Kuweka jiwe la msingi Maktaba ya Shule ya Sekondari Mangamba • Kuona maonesho ya wana sayansi chipukizi • Kugawa taulo za kike kwa wanafunzi wanaoishi mazingira magumu.	DC
	10:00 -10:10	Mnarani	6.2	Msafara kuelekea uwanja wa Mashujaa	
	10:10	Uwanja wa Mashujaa		• Kuona na kukagua mabanda mbalimbali kwa ajili ya shughuli za mapambano dhidi ya o dawa za kulevya, o Rushwa, o VVU/UKIMWI, o Malaria • Kukagua banda la VETA/VSO • Kugawa zawadi ya pikipiki kwa Kata iliyoongoza kwa Usafi. • Kugawa hati za urasimishaji wa viwanja kwa wananchi • **Risala ya Utii** • **Ujumbe wa Mwenge**	

				• Mkesha wa Mwenge	
	12:00-01:00	Tiffany Diamond		Chai	DC
	01:00-01:45	Uwanja wa Mashujaa		Kuwaaga wananchi	DC
	01:45-2:30	Uwanja wa Mashujaa	48.3	Msafara kuelekea Madangwa – Lindi	
	02:30-03:00	Madangwa-Lindi		Makabidhiano ya Mwenge na uongozi wa Mkoa wa Lindi	RC Mtwara/RC Lindi
			90		

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MKOANI MTWARA

11/06/2018	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu
12/06/2018	Halmashauri ya Mji Masasi
13/06/2018	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi
14/06/2018	Halmashauri ya Mji Newala
15/06/2018	Halmashauri ya Wilaya ya Newala
16/06/2018	Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba
17/06/2018	Halmashauri ya Mji Nanyamba
18/06/2018	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara
19/06/2018	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani

"ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA; WEKEZA SASA KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU"